# Mwongozo wa Mzazi Kuwasaidia Watoto Kukuza Maadili



KENYA INSTITUTE OF CURRICULUM DEVELOPMENT

*A Skilled and Ethical Society*

Maadili ni misingi inayo elekeza watu katika hali ya maisha ya kila siku kama yanayofaa au yasiyofaa. Hueleekeza mienendo yetu, maamuzi yetu, matendo yetu na fikira zetu kwa yanayofaa maishani.

## Maadili huwasaidia watoto:

a) kuendeleza tabia njema

b) kuishi vyema na wengine

c) kuwa na nidhamu

d) kutatua matatizo


e) kukabiliana na ushawishi mbaya

f) kufanya maamuzi

## Mambo ya kuzingatia katika ukuzaji wa maadili

### 1 Upendo

- Kuweka maslahi ya wengine kabla ya yake binafsi
- Kujijali na kuwajali wengine
- Kusamehe kwa urahisi anapokosewa
- Kuepuka kuumiza wengine



### 2 Heshima

- Kuonyesha unyenyekevu
- Kusikiliza maoni ya wengine
- Kusubiri zamu yao katika shughuli mbalimbali na wenzao
- Kuwaelewa na kuwathamini wengine



### 3 Umoja

- Kufurahia kufanya kazi na wengine
- Kufanya kazi kwa malengo ya pamoja
- Kuheshimu mawazo na hisia za wengine
- Kugawana walicho nacho na wengine



### 4 Uwajibikaji

- Kutunza vitu vyao na vya wengine
- Kumaliza kazi waliyopewa
- Kuweza kutegemewa
- Kutatua matatizo bila kuwalaumu wengine



## 5

**Amani**



- Kuwa mtulivu
- Kuishi vyema na wengine
- Asiyependa kuumiza wengine
- Kutatua migogoro kwa njia ya utulivu

## 6

**Uadilifu**



- Kuchagua kufanya jambo linalofaa kila wakati
- Uaminifu na haki
- Kufuata kanuni wanapofanya mambo
- Kutumia rasilimali kwa njia inayofaa

## 7

**Uzalendo**



- Kuhudumia jamii
- Kutii sheria/kanuni
- Kupenda nchi yao
- Kuheshimu tamaduni mbalimbali

## 8

**Haki za Kijamii**



- Kuishi kwa maelewano na wengine
- Kutenda haki kwa kila mtu
- Kutoa fursa sawa kwa kila mtu
- Kutoonyesha upendeleo kwa yeyote

## Jinsi ya kubaini kama mtoto anatekeleza maadili:

- Kusikiliza jinsi mtoto anavyozungumza na wengine.
- Kusikiliza majibu ya maswali anayoulizwa mtoto.
- Kuangalia kama mtoto anaweza kueleza alichojifunza kutoka kwenye hadithi.
- Kumuuliza mwalimu kuhusu maongezi na matendo ya mtoto wako shuleni.
- Kuangalia mambo ambayo mtoto wako hufanya pamoja na marafiki zake.
- Kuchunguza kama mtoto wako hutimiza majukumu yote anayopewa.
- Kuangalia kama mtoto wako ako huru wakati anapozungumza na wewe.
- Kujua jinsi mtoto wako anavyotangamana na wengine.

# Jinsi ya kumsaidia mtoto kukuza maadili

## Kukuza Maadili

1. kuwa kielelezo chema kwa mtoto wako
2. kuweka sheria nyepesi kama vile kuheshimu wengine
3. kumrekebisha mtoto wako kwa upendo
4. kumpa mtoto wako kazi kulingana na umri wake
5. kumshirikisha mtoto wako katika kufanya maamuzi katika mambo yanayomhusu
6. kuhimiza mazoea ya kifamilia kama vile kula pamoja
7. kupongeza na kutambua tabia njema
8. kusimuliana hadithi zenye mafunzo ya kimaadili
9. kumpa mtoto wako uhuru wa kuzungumza na wewe bila uwoga
10. kuhudhuria mikutano ya wazazi, na ya masomo shuleni
11. kuweka picha zenye maadili kwenye ukuta
12. kumsaidia mtoto wako kufanya kazi za shuleni

## Nani anapaswa kumsaidia mtoto kukuza maadili?

